# Mitaala ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki

# 12

# Fasihi ya Watoto katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki

Pamela NGUGI

## Utangulizi

Utafiti uliofanywa na shirika la Uwezo - Kenya kuanzia mwaka wa 2014 hadi 2016 kuhusu "Are our Children Reading?" umethibitisha kuwa watoto wengi hasa katika shule za msingi hawajui kusoma na kuandika kwa mujibu wa viwango vya madarasa waliyomo. Kwa sababu hiyo, shirika hili limependekeza mabadiliko katika ufundishaji na kupendekeza kutumika kwa mkabala jumuishi wa elimu iwapo sekta ya elimu inatarajia kupata maendeleo thabiti. Mkabala jumuishi huhimiza wanafunzi kushiriki katika ujifunzaji wao na hivyo basi, kusaidia katika ukuzaji wa maarifa ya kufikiria kwa kiwango kikubwa. Katika kufanya hivi, ujifunzaji huwa wa maana kwa mwanafunzi na huchangia katika kujenga stadi nne za lugha ambazo ni: kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika, kusikiliza na kuongea kwa kiwango cha juu.

Lengo la makala hii ni kujadili na kubainisha namna ambavyo fasihi ya watoto inaweza kutumika kama kichocheo cha kujua kusoma na kuandika, hasa pale ambapo wanafunzi wanapewa nafasi ya kujenga maana kutokana na usomaji wao. Fasihi ya watoto inaweza kuchangia katika kuinua maarifa, stadi na milelekeo chanya miongoni mwa wanafunzi kuhusiana na masuala ya kusoma na kuandika hali ambayo itachangia katika kufikia lengo la 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu katika sekta ya elimu kuhusiana na kuhakikisha

kuwa watoto wanapata elimu bora na yenye usawa kwa wote na kutoa fursa kwa wote kujiendeleza (UN, 2015) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## Fasihi ya Watoto katika Elimu

Fasihi ya watoto hutumika kujenga msingi wa ufahamu na kuwachochea wanafunzi wakati wa kujifunza. Matumizi ya Fasihi ya Watoto kufundishia yamepata uungwaji mkono katika siku za hivi karibuni. Hii inatokana na umuhimu wa fasihi ya watoto kutumika katika mafunzo ya tabia za vijana. Hivyo basi, fasihi ya watoto ni rasilimali muhimu sana katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Katika makala hii, maana ya Fasihi ya Watoto inachanganuliwa na kuonyeshwa kinadharia namna inavyoweza kutumiwa kufundisha wanafunzi wa Vyuo vikuu. Hili linawezekana kwa kuwa lugha ni mche ambao binadamu hutumia kuupa maana ulimwengu unaowazingira.

Kwa mujibu wa Kembo (2016) kupitia lugha tunaweza kujua kusoma na kuandika. Lugha ni muhimu katika kuhakikisha kuwa kila mwanajamii ameshiriki katika shughuli za kijamii kama msemaji, msikilizaji, msomaji na mwandishi. Kwa sababu lugha ndio uti wa mgongo wa mawasiliano, panahitaji kuwa na mikakati ya kuhakikisha kuwa wanajamii wote wanapata mbinu za kuwawezesha kushiriki katika masuala mbalimbali ya kijamii. Lugha ni chombo ambacho binadamu hutumia katika kuwasilisha hisia zake, fikira zake na matamanio yake kwa wanajamii wengine.

Utafiti wa Shirika la Uwezo- Kenya (Uwezo Kenya, 2016) umeonyesha kwamba kusoma na kuandika ndizo stadi za kimsingi na nguzo za maendeleo katika jamii. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni madai mengi yametolewa kuhusu kiwango cha welewa wa wanafunzi wa shule za msingi nchini Kenya. Tatizo kuu likiwa kwamba baadhi yao hawawezi kusoma vitabu vya viwango vya chini mno. Mara

nyingi suluhu zinazopendekezwa zimehusu uongezaji wa vitabu vya kusoma shuleni pamoja na kubadilisha mbinu za ufundishaji wa masomo ya lugha. Hata hivyo, viwango vya kusoma na kuandika vimeendelea kudorora. Hali hii inahitaji kufanyiwa utafiti wa kina na vyuo vikuu pamoja na kuandaa mitaala ambayo inaweza kuwaandaa wanafunzi vilivyo. Makala hii inajikita kwenye fasihi ya watoto kama mojawapo ya mbinu za kuwandaa wanafunzi kujifunza kusoma na kuandika.

## Nadharia ya Utanzu wa Fasihi ya Watoto

Miller (1984) na Devitt (1993) wanasema kwamba utanzu ni aina na namna fasihi inavyokabiliana na uhalisi wa jamii. Nadharia ya fasihi ya watoto inaeleweka kutokana na sifa maalum zinazoitambulisha na kuitofautisha na tanzu nyingine. Muktadha wa mwandishi ndio husababisha kuibuka kwa tanzu za fasihi. Kila utanzu una kanuni zake ambazo zinahitaji kuzingatiwa wakati wa kusoma. Hata hivyo, watunzi mara kwa mara hutumia na kuchanganya sifa na kanuni mbalimbali ili kubuni mtungo wenye mvuto zaidi. Fasihi ya watoto ndio utanzu pekee ambao, tofauti na tanzu nyingine, hutambuliwa kwa kuzingatia hadhira – watoto.

Aghalabu fasihi ya watoto hufikiriwa na kueleweka kwa misingi ya dhima ya burudani, badala ya kuitazama kama chombo cha kufunza maadili. Ingawa vitabu, mashairi na michezo katika fasihi hii huwalenga watoto, si nadra kupata watu wazima nao wanaisoma na kuifurahia. Hii ndiyo maana Makala hii inaonelea kuwa fasihi ya watoto inastahili kuzingatiwa kwa makini katika mitaala ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki.

Kabla ya karne ya kumi na tisa, tungo chache ziliandikwa kwa ajili ya watoto. Baada ya mitazamo kuwahusu watoto na maendeleo yao katika jamii kuanza kubadilika na suala la kuwatambua kuwa muhimu, fasihi ya watoto imekuwa

ikikua kwa kasi huku ikinufaika kutokana na TEHAMA. Lakini kama ambavyo dhana za 'mtoto', 'utoto' na 'fasihi' zimekuwa zikibadilika, ndivyo ambavyo maana na maelezo ya 'Fasihi ya Watoto' nayo imekuwa ikibadilika.

Kuna wataalamu kama vile Lukens (1995) ambao wanadai kuwa fasihi ya watoto inatofautiana na fasihi ya watu wazima kwa viwango pekee, ilhali wachunguzi wengine kama vile Lesnik-Oberstein (1996) kwamba tofauti inajitokeza kwa fani na maudhui. Ni kutokana na hali hii ambapo Hodder na Bottigheimer (1998) wanasema ni vyema kuielewa fasihi ya watoto kuwa sanaa na mfumo kamili na huru. Mbali na ukamilifu wa kujieleza, Hillman (1999) anapendekeza kwamba fasihi ya watoto iwe na ubora wa kisanaa.

Licha ya mitazamo tofautitofauti kuhusu maana ya fasihi ya watoto, wataalam wengi wanaelekea kukubaliana kwamba hadhira lengwa ni kigezo cha kimsingi katika ufafanuizi. Fasihi hii huwalenga watoto ambao wanatambuliwa kwa misingi ya sifa za kijamii, kitamaduni na kibinafsi (taz. Galda & Cullinan, 2002; Hunt, 1996; Lesnik-Oberstein, 1999; McDowell, 1973; Weinreich & Bartlett, 2000). Wataalamu hawa wanadai kwamba katika kubuni fasihi ya watoto, ni lazima mtoto awe ndiye mlengwa mkuu, na ikibidi hilo litajwe wazi na mwandishi. Kwao, fasihi ya watoto ni mtungo wowote ambao umeandikiwa watoto: maudhui yanawalenga, na ndio hadhira inayokusudiwa kuusoma. Watoto ni kundi maalumu katika jamii yoyote ile na ndio walengwa wa fasihi ya watoto.

Hata hivyo, ufafanuzi wa fasihi ya watoto kwa kujikita kwenye kigezo cha hadhira kunasababisha changamoto kadhaa. Kwa mfano: kuna watoto ambao husoma fasihi ambayo haikuandikwa kuwalenga wao kama hadhira yake.

Mbali na kigezo cha hadhira, fasihi ya watoto pia imefafanuliwa kwa kuzingatia azma ya maudhui yanayotolewa na dhima ya burudani Norton, 1999; Tomlinson & Lynch-Brown, 1996/2002; Winch, Johnson, March,

Ljungdahl & Holliday, 2004). Wafuasi wa mtazamo huu wanaamini kuwa fasihi ya watoto inalenga kuwafundisha kujifunza kutokana na hali maishani na kukua kwa misingi mizuri ya maadili pamoja na kuweza kuwajali watu wengine katika jamii (Huck, Helper, Hickman & Kiefer, 2001; Saxby, 1997;Tomlinson & Lynch-Brown, 1996/2002).

Kwa mujibu wa Lukens (1995), kuna wachunguzi ambao husisitiza haja ya kuifafanua fasihi ya watoto kwa misingi ya mtindo na ubora wa ubunifu kisanii. Katika msingi huu, fasihi ya watoto inatarajiwa kwa lugha iliyo muafaka na inayoeleweka kwa urahisi.

KENYATTA UNIVERSITY RECEIVED 1 NOV 2019 KISWAHILI & AFRICAN LANGUAGES P.O. Box 43844-00100 NAIROBI

Kimsingi, fasihi ya watoto huchukuliwa kuwa ni tungo za kisanaa zenye ubunifu unaokusudiwa kuwaburudisha na kuwafundisha watoto. Hollindale (1997) anasema fasihi ya watoto iweze kuibua hamu wakati inaposomwa na watoto. Maoni haya ni sawa na ya Ghosn (2002) anayefafanua kuwa fasihi ya watoto ni mtungo unaosimuliwa ili utoe burudani zaidi kwa msomaji kuliko mafundisho. Galda na Cullinam (2002) wanashikilia kwamba fasihi huburudisha na hufundisha; hivyo fasihi ya watoto nayo hupanua mtazamo wao kuhusu ulimwengu wao. Kupitia fasihi hii, watoto hujifunza kuhusu watu na maisha yao katika jamii. Fasihi hii hujenga hisia za watoto, mitazamo yao, maadili na jinsi ya kuishi katika ulimwengu. Hili hufanikishwa kupitia kusoma na kuona tajriba za watu wengine katika jamii.

Kutokana na sifa yake ya kiusimulizi, fasihi ya watoto haijulikani ilianza lini. Kwa muda mrefu, jamii nyingi zilitumia ubunifu kuwalea watoto na kuwajengea maadili. Hivyo, inaweza kudaiwa fasihi ya watoto ni kongwe kama zilivyo jamii. Kile ambacho kimebadilika ni mfumo na muundo wa fasihi hii. Kazi za John Locke kuhusu nia na mawazo ya watoto ndizo ambazo zilijenga msingi wa kuanza kuwatazama watoto kama binadamu maalumu waliohitaji kushughulikiwa kama kundi maalumu katika jamii.

Karne ya kumi na tisa inachukuliwa kuwa kipindi ambamo fasihi ya watoto ilistawi na kunawiri. Juhudi za awali za John Newbery za kuchapisha *Newbery's Pretty Pocket Book* mnamo 1744 kwa ajili ya mafundisho na burudani na uamuzi wa kutenga sehemu maalumu iliyochapisha vitabu vingine vya fasihi ya watoto. Baadaye maendeleo ya kijamii ikiwa ni pamoja na viwanda na mifumo ibuka katika kipindi hicho, fasihi ya watoto ilinawiri. Kwa sasa, fasihi ya watoto imetanuka na hujitokeza katika miundo mbalimbali kuliko kipindi kingine cha hapo awali. Teknolojia imechangia ukuaji huu wa kasi wa fasihi ya watoto. Fasihi hii sasa hupatikana katika tanzu za aina kwa aina na hata maudhui yake ni pana na ya kina.

Kwa ujumla basi, fasihi ya watoto ni utanzu ambao unafafanuliwa kutegemea vigezo mbalimbali. Hata hivyo, mhimili mkuu katika kuelezea fasihi ya watoto ni uzingatiaji wa hadhira lengwa ambao ni watoto, pamoja na hali, mahitaji na matarajio yao. Hii ndiyo maana Tomlinson & Lynch-Brown (2002) wanasema kwamba ni muhimu fasihi ya watoto ihusishe *tungo zozote* ambazo zinawajali watoto wa umri tangu kuzaliwa hadi kubaleghe. Tungo hizo ni pamoja na drama, ushairi, riwaya, wasifu, tawasifu na simulizi nyinginezo. Hata maandishi ya kifalsafa, historia na sayansi ambayo yanatimiza vigezo vya maudhui na fani yanaweza kuwa fasihi ya watoto (Winch, n.w; 2004). Winch, n.w; (2004) wanasema fasihi ya watoto ni muhimu sana katika kufundisha elimu ya lugha, hasa stadi za kuongea na kusikiliza. Katika makala hii, hoja muhimu ni kwamba fasihi ya watoto ina nafasi katika mitaala ya Kiswahili ya vyuo vikuu vya Afrika Mashariki.

## Nafasi ya Fasihi katika Kukuza Mbinu na Stadi Maishani

Fasihi ya watoto ina nguvu ya kukuza mbinu za Kiisimu, na za uhusiano wa Kihisia- kijamii (socio- emotional skills). Kwa mujibu wa Collie na Slater (1992) na Ngugi (2014), fasihi

huwakilisha matumizi mbalimbali ya lugha ambayo ni ya kimazoea na kifasihi, pia hudhihirisha mikakati mbalimbali ya mawasiliano kuliko inavyopatikana katika mbinu zozote za ufundishaji wa lugha, na hivyo basi hutoa ujuzi wa kiisimu kwa mapana katika viwango vya matumizi. Wanafunzi wanaposoma fasihi, huwa wanajifunza lugha lengwa katika muktadha mzima kuliko kule kukariri maneno na sheria za lugha hiyo. Mbinu hii ya kupokea lugha inafanana na ile harakati ya kupata lugha pasipo kusomeshwa kirasmi (Chen, 2006).

Tofauti na ujifunzaji wa misamiati na miundo ya lugha inayofanyika kirasmi darasani, fasihi hutoa mazingira asili na yasiyo rasmi lakini yanayochangia katika kuendeleza mbinu za kiisimu. Vile vile Chen (2006), anasisitiza kuwa utumiaji wa fasihi katika kufunza lugha ni njia moja ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaojifunza lugha fulani wanapata nafasi ya kukutana na mzungumzaji (ambaye ni mwandishi wa kazi hiyo) wa lugha hiyo ndani na nje ya darasa. Fasihi hivyo basi, huwa na uamilifu wa aina mbili, kwanza inafanya kazi kama pembejeo (input) kwa sababu inawasilisha lugha kama mawasiliano halisia; kama *output*, inaweza kuwa kichochezi cha kuwahamasisha wanafunzi kujadiliana na kuandika matini zao (Chen, 2006).

Naye Widdowson (1983), anasema kuwa fasihi hutoa vikwazo vilivyo muhimu katika ujifunzaji wa lugha yaani hujenga ule uwezo wa kufahamu maana kutokana na mazoea ya kusoma. Vilevile, Chen (2006) anasema kuwa fasihi hujenga mbinu za kusikiliza hasa inapotolewa kimasimulizi kwa sababu huhimiza mazungumzo kupitia kwa mijadala na hutoa nafasi kuntu ya kuandika. Katika kusisitiza hoja hii Leal, (2015) anaeleza kuwa baada ya kusoma kitabu fulani cha fasihi, wanafunzi wanaweza kuanza kwa kutambua maneno magumu wasiyoyafahamu huku wakijaribu kueleza maana za maneno hayo. Katika harakati hii, watakuwa wakichangiana-bila ujuzi wao wa maneno mbalimbali papo hapo watakuwa

wanajifunza maana za maneno kutoka kwa wenzao katika mazingira tulivu. Muhimu ni kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anachangia katika mjadala wa darasani na pia kila mmoja wao anapata kujifunza kutoka kwa mwenziwe na pia kila mmoja anakuwa mwanafunzi wa mwenzake. Baada ya kutambua maneno haya, orodha ya maneno hayo inaweza kutolewa kwa makundi mbalimbali ya wanafunzi, kisha kuwataka wanafunzi kuunda sentensi mbalimbali kwa kutumia maneno hayo. Wanafunzi walio na umilisi wa kiwango cha chini wanaweza kujumuishwa pamoja na wale wa umilisi wa juu ili kushirikiana katika kuunda sentensi mbalimbali darasani.

Fasihi ya watoto inaweza kutumiwa kama modeli ya uandishi kutokana na wanafunzi kubuni upya hadithi waliyopewa wakitumia msamiati wa hadithi asilia. Hii ina maana kuwa muundo wa matini, sarufi na msamiati wa hadithi asilia unachukuliwa na kutumiwa na wanafunzi wanapoandika hadithi zao. Hivyo basi, kama pembejeo (input), fasihi huwasilisha aina mbalimbali ya lugha ya mawasiliano kwa mwanafunzi lakini iliyo asilia na kwa sababu hiyo, inaweza kuwachochea wanafunzi katika mijadala na pia kutoa nafasi ya kuandika. Hivyo basi, mbinu amilifu za lugha zinakuzwa katika miktadha halisi ya mazungumzo. Kwa kuzingatia msimamo wa kiisimu, tunaweza kudai kuwa kutokana na kuwapa wanafunzi vitabu anuwai vya kusoma, tutakuwa tunawatanguliza kwa mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha.

Wakati wa mazoezi ya ufahamu darasani, wanafunzi wanaweza kupewa nafasi ya kujitungia maswali ya ufahamu badala ya kuegemea tu kwa mtindo wa kijadi wa kuulizwa maswali ya ufahamu (Leal, 2015). Mbinu hii ya kupima uwezo wa kusoma, harakati ya kuichanganua na kuelewa maana ya matini huweza kuwasaidia wanafunzi kuzama zaidi katika usomaji wao (Collie & Slater, 1992). Kupitia kwa mbinu hii, wanafunzi wanapewa nafasi ya kutoa maoni yao, hisia zao

pamoja na kuhusisha tajriba zao binafsi na za kitamaduni dhidi ya zile zilizotolewa katika matini. Modeli hii huwasaidia wanafunzi kupata maarifa kupitia maudhui mbalimbali yaliyopo kwenye matini pamoja na kusaidia katika kuendeleza lugha yao. Uamilifu huu unaingiliana na mtazamo wa mwitikio wa msomaji wa Rosenblatt (1995). Rosenblatt (keshatajwa) anahoji kwamba usomaji ni mapatano yanayohusu msomaji kuvyaza maana ya kifasihi kutokana na kazi anayoisoma au kuisikiliza. Kwake yeye, mapatano haya yanadhihirika kwa njia mbili kuu: maarifa na ujumi.

Njia ya ufanisi inahusu kule kupata maarifa au taarifa fulani baada ya kusoma kazi ya kifasihi. Aina ya pili ya mapatano yanahusu ujumi wa kifasihi. Ujumi wa kifasihi hujumuisha mambo kama vile kufikiria, kuhisi na kupata tajriba ya kifasihi kutokana na kazi anayoisoma. Njia hii ya pili inalenga hali ya kutambua jinsi vipengele tofauti vya kifasihi kama vile fani na maudhui vinavyoingiliana na kuchangia katika kujenga umoja na ukamilifu wa kiumbuji wa kazi ya kifasihi. Namna hizi mbili za usomaji hudhihirika kwa njia ya kimwendelezo. Hii ina maana kuwa hakuna mpaka kamilifu kati yazo wakati shughuli ya usomaji inapoendelea. Kile kinachotokea ni kwamba harakati hizi hubadilishana nafasi kulingana na namna msomaji anavyosoma (Pennell, 2014 katika Ngugi 2016).

Kulingana na Rosenblatt (1995), matini inayosomwa huwa ni kichochezi kinachoibua tajriba mbalimbali za zamani, fikra na hata mawazo kutoka kwa msomaji, inayotokana na hali za kawaida za maisha au hata tajriba kutokana na usomaji wa awali. Miitikio hii huathiri jinsi msomaji anavyoelewa matini katika usomaji. Hii ina maana kuwa msomaji anapoendelea kusoma, ile matini huwa kama mpango- makini (blue print) unaoweza kutumika ili kudhibiti ufasiri uliokithiri anapogundua kuwa ufasiri wake umeenda nje ya kile kilichomo kwenye matini (Rosenblatt, 1995). Kwa njia hiyo hiyo basi inaweza kudaiwa kuwa ujifunzaji umefanyika pale

ambapo wanafunzi wanapoweza kufasiri matini na kupata maana kwa misingi ya tajriba zao. Vivyo hivyo, wanafunzi wanapojadili matini huku wakielekezwa na msomaji aliyekomaa huwa wanatambulishwa kwenye miundo mbalimbali ya matini na jinsi inavyoafiki malengo mbalimbali ya kijamii. Vile vile, wanafunzi wanapata kufahamu aina mbalimbali za tajriba ziwe halisi au za kiubunifu pamoja na kujua tofauti zilizopo kati ya lugha andishi na lugha ya mazungumzo.

Leah (2015), anabainisha dhima nyingine ya fasihi ya watoto kuwa ni kujenga uhusiano miongoni mwa wanafunzi kupitia mijadala endelevu ya darasani. Hili hutokea wakati mwalimu anapomhusisha mwanafunzi moja kwa moja katika usomaji. Wanafunzi wanaweza kujadiliana mambo mbalimbali miongoni mwao pamoja na kupokea maoni ya wenzao. Katika kufanya hivi, watakuwa wanapanua mitazamo yao kuhusiana na mwonoulimwengu wao. Mbinu hii humpa mwanafunzi kipaumbele katika mchakato wa ujifunzaji kwa kumshirikisha kimtagusano kwenye ngazi za upataji, uhusisho, ufanisi na utumiaji wa maarifa katika utatuzi wa mambo yanayomhusu kwenye mazingira yake (Republic of Kenya, 2017). Kuptia kwa mbinu hii wanafunzi wanaweza kusaidiana, kujifunza kutoka kwa wenzao na mwishowe kujenga ujamaa miongoni mwao (Leah, 2015). Wanafunzi wanapohusishwa kwenye mijadala ya darasani, huwa wanapata ujasiri wa kutumia lugha jambo ambalo litawapa ukakamavu na hivyo basi kuwajenga kibinafsi.

Kwa hakika mikabala hii mitatu ya kufunza fasihi hutofautiana tu kulingana na jinsi makala yanavyoangaziwa. Katika mkabala wa kwanza, msisitizo upo kwenye uchanganuzi wa miundo ya kisarufi,; mkabala wa pili unaangazia makala kwa njia ya kujenga mwanafunzi kiutambuzi na kiutafakari, na mtazamo wa tatu unahusu namna ya kumsaidia mwanafunzi kujenga uhusiano na wenzake darasani. Mkabala unaojumuisha vipengele hivi vyote katika

somo la fasihi utachangia katika kumkuza mwanafunzi kiisimu, kiutambuzi na kiutafakari pamoja na kimahusiano.

## Umuhimu wa Fasihi ya Watoto katika Mitaala ya Kiswahili ya Vyuo Vikuu

Norton (2010) anadai kuwa kufundisha Fasihi ya Watoto kunaweza kumfanikisha msomaji maishani. Hivyo basi, wazazi, walimu na jamii hawana budi kutilia maanani Fasihi ya Watoto na kuhimiza ufundishaji wake. Kuna sababu kadhaa zinazoonyesha umuhimu wa fasihi ya watoto kwa jamii. Sababu hizo zinaafikiana na malengo, dhima, Imani, matarajio na stadi za elimu ya fasihi ya watoto. Fasihi ya Watoto ni utanzu ambao bado haujaendelea sana katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo, kuanzishwa kozi ya Fasihi ya Watoto kuna umuhimu kwa fasihi ya Kiswahili kwa sababu kunachangia ukuaji wa fasihi hii.

Kwanza, Fasihi ya Watoto hutoa fursa kwa wanafunzi kusoma na kuelewa utamaduni wao na wa watu wengine katika jamii. Ukuaji katika jamii na ufanisi maishani ni mambo yanayotegemea utamaduni wa mtu binafsi na utamaduni wa watu wengine. Utamaduni ni rasilimali muhimu ya jamii kujiendeleza. Kwa kusoma vitabu hivyo, wanafunzi watapenda utamaduni wao na kuwa tayari kuchangia ujenzi wa taifa.

Pili, Fasihi ya Watoto huwasaida wanafunzi kuwa wabunifu na kujijengea ufahamu unaohitajika kuielewa jamii na mabadiliko yake. Kuna mambo na matukio mengi katika jamii ambayo yanahitaji vijana na wanafunzi kutumia akili zao kukabiliana nazo ili kuzitatua. Kupitia kusoma Fasihi ya Watoto, mwanafunzi anajifunza maisha yalivyo, changamoto zake, pamoja na jinsi ya kuzitatua.

Tatu, Fasihi ya Watoto hukuza vipawa vya wanafunzi na stadi za kimaisha. Kwa mfano, Fasihi ya watoto ina hadithi na visa ambavyo vinaonyesha migogoro na jinsi ya kuitatua.

Kwa kusoma kazi hizo, wanafunzi wanaelewa jinsi ya kukabiliana na hali mbalimbali katika maisha yao pamoja na migogoro inayojitokeza.

Nne, Fasihi ya Watoto huhifadhi na kupitisha maudhui muhimu kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Tano, wanafunzi wanapata fursa ya kujiendeleza na kutoa maoni juu ya mitazamo yao kuhusu fasihi katika jamii.

Sita, Fasihi ya Watoto huwasaidia wanafunzi kuona uhalisia wa maisha na tofauti zake. Wanafunzi wanaposoma Fasihi ya Watoto wanakubali kuwa duniani kuna watu wa aina mbalimbali na kwamba tofauti kama vile za kijinsia, kielimu, rangi, kimaumbile na nyinginezo ni sehemu ya maisha ya binadamu.

Saba, ni muhimu kufundisha Fasihi ya Watoto ili kuwapa wanafunzi wa Kiswahili katika vyuo vikuu fursa ya kukabiliana na upya katika fashi ya Kiswahili.

Nane, Fasihi ya Watoto ni muhimu kwa kuwa inatoa msingi mzuri kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kuweza kuwaelewa watoto kwa undani, na kujenga taswira kamili ya kipindi cha ukuaji ambamo watoto hupitia. Mtaala kuhusu kundi hili muhimu la kijamii unastahili kwani unawafahamisha watu majukumu yao katika kuwalea watoto kwa kuwapatia mafunzo ya namna ya kuishi katika jamii kwa kuwa na uhusiano mzuri na watu wengine. Fasihi ya watoto inaweka msingi wa kujenga utu, uzalendo na utaifa.

Tisa, kozi ya Fasihi ya Watoto inamsaidia mwanafunzi kusoma tungo pevu za aina mbalimbali ambazo huwa zimetungwa katika mazingira na miktadha tofautitofauti. Hali hii inamwezesha msomaji kuelewa hofu na matarajio ya jamii kwa watoto.

Kumi, tungo kwa ajili ya watoto inawafundisha wanafunzi na hivyo kuwaathiri kwa njia kubwa. Msomaji anapata kuelewa masuala ya kihistoria, kisosholojia, kisaikolojia na kijamii kuhusu watoto na ukuaji wao.

## Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki

Fasihi ya Watoto ni rasilimali ya kufundisha ujenzi wa elimu ya tabia nzuri maishani. Fasihi ya Watoto inaweza kufundisha masuala mengi sana katika jamii (Auciello, 2006; Clare & Gallimore, 1996; O'Sullivan, 2004; Smith-D'Arezzo & Moore-Thomas, 2010; Prestwich, 2004), ikiwa ni pamoja na yale yanayowahusu wanafunzi darasani na hata nje (Jalongo, 2004; Lowe, 2009). Ni kutokana na umuhimu huu pamoja na mchango wake ambapo makala hii inapendekeza kwamba Fasihi ya Watoto ifundishwe kwa wanafunzi wa Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki.

Mbinu ya kufunza stadi za lugha kwa kuegemea kwenye fasihi ni suala ambalo limewahusisha wataalamu mbalimbali wa elimu (Kama vile Hiebert na Colt, 1989; Tunnell na Jacobs 1989; Zarillo 1989; & Leal 2015) hasa kutokana na kutaka kujua mbinu hii inahusu nini na ina manufaa gani katika elimu. Kwa mujibu wa Hiebert and Colt (1989), ufundishaji wa kusoma kupitia fasihi unahusu programu nzima ya usomaji ambayo inajumuisha mwingiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi pamoja na uteuzi wa vitabu vya fasihi ambavyo vinaweza kumsaidia mwanafunzi katika kujijenga kama msomaji-mtafakari. Tunnell na Jacobs (1989) nao wanaeleza kuwa mbinu hii ni mchakato ambao, kimsingi hutumia vitabu vya "kihalisia" kufunzia na kuendeleza kujua kusoma na kuandika.

Naye Zarillo (1989) anahoji kuwa mbinu za ufundishaji wa kusoma kupitia fasihi ni matendo yanayohusishwa na shughuli mbalimbali kwa kutumia riwaya, vitabu vya arifa, hadithi fupi, mashairi na tamthilia. Anasisitiza kuwa fasihi hii isiandikwe upya kwa minajili ya kufunzia na kwamba ichukue mahala pa vitabu vya kiada wala si kufanya kazi ya ziada ya usomaji darasani. Kwa ujumla, dhana hii inarejelea hali ya kutumia vitabu vya fasihi katika kufundisha

lugha na kwa lengo la kuendeleza stadi ya usomaji (Leal, 2015). Katika kufanya hivi, watoto watahusishwa katika usomaji na wataweza kutumia lugha kiuamilifu.

Rasimu ya Mtaala mpya wa Elimu ya Msingi nchini Kenya (Republic of Kenya, 2017) imebaini vipengele vya umilisi anavyostahili kuzingatia mwanafunzi ili kuimarisha utendaji wake katika ujifunzaji na utatuzi wa mambo. Rasimu hii inatokana na mchakato wa kufanyia mabadiliko mtaala wa elimu ya msingi kukidhi mahitaji ya jamii katika karne ya ishirini na moja. Mtaala wa Kiswahili uliofanyiwa marekebisho mwaka 2002 ulikusudia kumpa mwanafunzi stadi nne za lugha zilizosawiri mada za kusikiliza na kuongea; masuala ibuka; sarufi na matumizi ya lugha; uandishi wa kiuamilifu; uandishi wa insha; fasihi na Isimujamii. Pengo kuu katika mtaala uliopo ni udhaifu wa mwanafunzi katika kuwasiliana kiuamilifu, kiadilifu na kwa kujiamini.

Rasimu ya Mtaala mpya imetaja kwa uwazi nadharia bunilizi za wanasaikolojia kama vile: John Dewey, Lev Vygotsky, Jean Piaget, Jerome Bruner, Erik Erikson na Gardner kuwa msingi wa kuelekeza Mitaala mipya. Kwa ujumla, nadharia bunilizi hizi humpa mwanafunzi kipaumbele katika mchakato wa ujifunzaji kwa kumshirikisha kimtagusano kwenye ngazi za upataji, uhusisho, ufanisi na utumiaji wa maarifa katika utatuzi wa mambo yanayomhusu kwenye mazingira yake. Mchakato huu mzima unafungamana na lugha anayotumia mwanafunzi kwenye ujifunzaji.

Kutokana na umuhimu wa lugha kama chombo cha kujieleza, makala hii inalenga kujadili na kubainisha namna ambavyo fasihi ya watoto inaweza kutumika kama kichochezi cha kujua kusoma na kuandika, hasa pale ambapo wanafunzi wanapewa nafasi ya kujenga maana kutokana na usomaji wao. Mapendekezo ya makala hii ni kuwa, fasihi ya watoto inaweza kuchangia katika kuinua maarifa, stadi na milelekeo chanya miongoni mwa wanafunzi kuhusiana na masuala ya kusoma na kuandika hali ambayo itachangia katika kufikia malengo ya

maendeleo endelevu katika sekta ya elimu katika jumuiya ya Afrika Mashariki.

Walimu wa Kiswahili katika vyuo vikuu wana wajibu wa kuteua na kupendekeza vitabu vinavyofaa kwa kufundisha Fasihi ya Watoto. Fasihi hiyo ijenge mtazamo wa kitaifa na kikanda kwa ajili ya kuwafanya wanafunzi waikubali nchi yao na kuikubali Jumuiya ya Afrika Mashariki. JAM ni eneo la kisiasa ambalo halina budi kueleweka kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ikiwa wanatarajiwa kuchangia utangamano na maendeleo endelevu.

Isitoshe, uteuzi wa vitabu ufanywe ili kuwawezesha wanafunzi wa vyuo vikuu kutambua na kuthamini mchango wa watoto na vijana katika JAM. Kundi hili ndilo lenye idadi kubwa katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika. Pia kundi hili ndilo ambalo linategemewa kuendeleza utangamano. Kwa sasa, nchi nyingi hazitambui na kuwajali sana watoto na vijana kuwa na umuhimu katika maendeleo na ujenzi wa taifa. Hii ni hali ambayo inahitaji kufanyiwa mapinduzi ya kimtazamo. Hivyo basi, fasihi ya watoto itakayofundishwa iweke msingi huo kwa ajili ya mafanikio ya baadaye. Watoto na vijana wakijiona katika fasihi, na pale wanapojihusisha na wahusika fulani katika kazi za kisanaa, kuna uwezekano mkubwa kwamba nao watajibiidisha katika kutekeleza wajibu wao katika jamii.

Kozi ya Fasihi ya Watoto inafaa kuandaliwa kwa namna ambayo itawasaidia wanafunzi kuelewa namna ya kujifunza na kuufundihsa utanzu huu. Hivyo basi, mbali na kujifunza kusoma tungo mbalimbali, ni muhimu pia kwa wanafunzi kuelewa jinsi ya kujitayarisha kusoma. Kwa mfano, fasihi ya watoto ina picha na michoro ambayo inasaidia katika kujenga maana. Ni muhimu maana hiyo ijulikane kabla na wakati wa kusoma fasihi ya watoto. Fasiri ya maana ya picha, michoro, rangi na mbinu nyingine zisizotumia maneno lakini zenye maana, ni mwanzo mzuri wa kuuelewa ulimwengu wa

fasihi ya watoto. Hivi ni vifunguo kwa maana ya ndani aliyoikusudia mwandishi.

Baada ya kusoma tungo mbalimbali, watoto wanatarajiwa kuzihusisha na hali katika Sanaa na uhalisia katika jamii. Kwa mfano, hadithi katika fasihi ya watoto inaweza kuhusu uchafuzi wa mazingira. Hadithi hii isisomwe tu na kufungwa katika mipaka ya mfumo husika. Mtoto asaidiwe kuihusisha hali inayochoorwa kwenye hadithi kitabuni na hali halisi katika jamii kuhusu haja na umuhimu wa kutunza mazingira. Dhana ya mazingira ielezwe kwa njia sahili ambayo itawafanya watoto kujua kwamba pale wanapokaa ni sehemu ya mazingira ya jamii.

Isitoshe, watoto wafundishwe namna ya kuhusisha wanachokisoma na maandishi na habari nyingine katika jamii. Kwa mfano, hadithi kuhusu bidi katika elimu inaweza kuhusishwa na habari hiyohiyo kwenye runinga, redio, magazeti, matangazo ya biashara, na nyimbo. Kwa kuhusisha maudhui katika fasihi ya watoto na hali halisi katika jamii kutasadia watoto kuwa wadadisi na wahakiki wa mambo. Pia, watoto watajenga uwezo wa kutafakari mambo na kujiimarisha kijamii (Ghosn, 2002).

Ufundishaji wa fasihi ya watoto ni suala ambalo linahitaji kutiliwa maanani kwa kuwa wataalam wamethibitisha mchango wake katika ukuaji wao pamoja na kusaidia kujifunza lugha kwa minajili ya mawasiliano mazuri katika jamii (Amspaugh, 1991; Barone, 1996; Altwerger, & Ivener 1994). Vitabu vizuri vya fasihi ya watoto vinafaa kuteuliwa na kutumiwa katika kufundisha. Vitabu hivyo vizingatie mambo kama vile maudhui, hadhira, malengo, wahusika, picha, michoro, rangi, usimulizi, mazingira, ploti, migogoro, na utatuzi wa tofauti zinazojitokeza (Tomlinson and Lynch-Brown, 2002; Hillel & Mappin, 1995; Stewig, 1980;).

Ili wanafunzi waweze kufaidika kutokana na fasihi wanayosoma, kuna umuhimu wa kuzingatia na kutilia maanani elementi za kimazingira kuhusu wasomaji kabla ya

kuwahusisha katika harakati ya usoamaji. Mazingira haya ni pamoja na umri, tabia za usomaji na aina ya wasomaji, viwango vya lugha, aina ya matini na urefu wake (Hafiz, 2002; Collie and Slater, 1992; Ngugi, 2014). Kwa mfano, Collie na Slater (keshatajwa) wanaeleza kuwa jambo la msingi linalohitaji kuzingatiwa ni iwapo kitabu kilichoteuliwa kinaweza kuwachochea wasomaji na kuwafanya wachangie katika mijadala darasani.

Watoto huwa na tajriba tofauti na finyu ikilinganishwa na ya watu wazima kuhusu maisha. Watu wazima huwa wanaweza kutambua mambo kutokana na kuyahusisha, kufikiria na vile vile uhisivu wao umekomaa kupitia tajriba mbalimbali maishani. Kwa upande mwingine, watoto hawana werevu na mbinu ambazo watu wazima wamechukua muda mrefu kuzipata. Ulimwengu wa watoto na mazingira yao hubainika kwa njia zisizoegemea kokote na vilevile huwa mawazo ya wengi wao yamejaa ujonzi. Kwa sababu hizi, uwezo wao unahitaji kuchukuliwa kwa makini wanapoteuliwa vitabu. Hivyo basi kitabu kinachomfaa mtoto ni kile kinachoweza kueleweka, kinachowavutia, kuwaburudisha na kuambatana na mahitaji yao ya kisaikolojia, (Ngugi, 2012, 2014).

Ili kuwateulia watoto vitabu vitakavyo wafaa, nadharia tete ya Pembejeo ya Krashen (1982 kama ilivyonukuliwa katika Ngugi, 2014) (Input Hypothesis) inahitaji kuzingatiwa. Krashen anasema kuwa kiwango cha kipembejeo cha ufahamu wa mwanafunzi kinahitaji kuwa i+1, ambapo i inarejelea hali ya sasa ya umilisi wa mwanafunzi na i +1 inawakilisha kiwango cha juu kidogo ambacho mwanafunzi anaweza kung'amua makala kutokana na viziada lugha na muktadha uliopo. Hii ina maana kuwa ile pembejeo isiwe sahili mno kiasi cha kuvunja motisha ya msomaji, au kisiwe kigumu sana kiasi cha kuzuia msomaji kuelewa matini.

Aguilera (1992 katika Ngugi 2012) amegawa wasomaji wa fasihi ya watoto kwa jumla katika makundi

matatu makuu: kikundi cha watoto wasiojua kusoma (0-6), wale wanaoweza kusoma (6+) na wale walio katika kiwango cha mpito wa maisha au waliobelehe na vijana. Tofauti katika makundi haya inatokana na ukuaji katika uwezo wa kuelewa au kungamua mambo ambayo hasa yanatokana na maarifa yao kuhusu ulimwengu. Utambuzi huu ni muhimu kwa sababu unawasaidia kufasiri mambo mbalimbali wanayokumbana nayo. Hivyo basi, wale walio katika umri wa chini watapata ugumu kuelewa mambo kwa haraka. Mipaka ya uanishaji si bainifu katika kiwango cha baada ya kubalehe kwa sababu shauku za kila mtoto ni tofauti. Ni rahisi kupata baadhi ya watoto katika kikundi fulani wakisoma fasihi ambayo imelenga kikundi kingine. Hii inatokana na sababu kuwa wasomaji huwa na mahitaji na tajriba tofauti.

Usomekaji au wepesi wa kusoma na vile vile uelewa ambao hutokana na ugumu wa mambo ya kiisimu, ni kipengele kimojawapo kinachohusiana na ufahamu wa makala. Suala la usomekaji hutegemea msomaji na mazingira ya usomaji (Puurtinen, 1998). Usomekaji pia huhusisha usemekaji . Hii inarejelea kwa ufaafu wa matini kuweza kusomeka kwa sauti na kwa mtiririko (Puurtinen, 1998). Hii ni sifa moja muhimu ya fasihi ya watoto kwa sababu mara nyingi vitabu vya watoto husomwa kwa sauti sio tu na watu wazima bali hata na watoto wenyewe. Hivyo basi mbinu ya kusikiliza huwa muhimu kwa mtoto ili aweze kupata anachosomewa. Kupitia kwa mbinu hii, mtoto huipokea hadithi na kuhusika nayo kwa hali ya juu. Kutokana na harakati ya usemekaji , msisitizo unahitaji kuwekwa kwa toni, mdundo, kiimbo na uwakifishaji ili hadithi iwe na mtiririko mzuri na imsaidie mtoto aweze kujenga picha ya hadithi akilini.

Urefu wa sentensi na utata katika sentensi ni baadhi ya vigezo vya kupimia usomekaji ingawa ni eneo ambalo limezua mjadala mkubwa. Kulingana na Puurtinen (1998) utata wa sentensi ndio huathiri sana usomekaji kuliko urefu wa sentensi. Matokeo ya makala isiyosomeka kwa mtoto msomaji

yaweza kuwa makubwa ikichukuliwa kwamba vitabu vinavyovutia na kufarahisha huwapa watoto motisha ya kusoma na kujenga tabia ya usomaji. Kwa upande mwingine vitabu vigumu na visivyoeleweka huweza kumtenga msomaji na hata kurudisha nyuma maendeleo katika ukuaji wa mbinu ya kusoma.


Michoro katika vitabu vya watoto huwa muhimu kwa sababu ni sehemu ya usomekaji na usemekaji na uwelewekaji wa makala. Michoro ni muungano wa vitu ambao umeundwa kutokana na maneno na picha na hutumia lugha maalumu. Hivyo basi vitabu hivi ni matinitaswira ambapo kuna mwingiliano kati ya usemezo na vielelezo, Oittinen (2008). Michoro huwa muhimu katika kumsaidia mtoto kuelewa hadithi kwa kuchochea dhana akilini. Michoro inayowekwa kwenye jalada huwa muhimu kwa sababu ndiyo elementi ya kwanza inayomvutia mtoto na kumpa shauku ya kutaka kusoma yaliyomo (Bakiza 2014).

Katika kuteua vitabu, ni muhimu kuzingatia vitabu ambavyo vitamsadia mtoto msomaji kuhusisha tajriba na hisia zao na kile wanachokisema (Rosenblatt, 1995). Hii ni kwa sababu wasomaji walio na mwelekeo chanya kuhusu kitendo cha usomaji au hata kuhusu usomaji wa kitabu fulani huenda wakasita kutumia tajriba zao za kifasihi wanapoisoma kazi husika. Hoja hii ni muhimu kutiliwa maanani hasa tunapowateulia watoto vitabu vya kusoma. Watoto watakuwa na mwitikio tofauti kutokana na ari waliyonayo kwa kitabu fulani. Vile vile mazingira wanamokulia, iwapo ni ya vitabu au la, yataweza kuathiri mwitikio wao kwa kazi ya fasihi. Ukweli ni kwamba bila kuwa na uelewa wa msomaji, hatuwezi kutabiri mielekeo watakayokuwa nayo kwa kitabu fulani (Rosenblatt, 1995).

## Mandalizi ya Somo katika Kipindi cha Fasihi ya Watoto

Mwalimu anahitaji kutayarisha mpangilio wa masomo ambao utawatayarisha wanafunzi kushiriki katika mijadala ya matini teule, kupata mtazamo wa mwandishi na kupata maoni kutoka kwa wanafunzi wengine. Mazoezi haya yanahitaji kutekeleza jukumu la kujenga mazingira faafu na yaliyo salama kwa wanafunzi hawa. Mazingira kama haya yanatoa nafasi kwa wanafunzi kupata tajriba ya pedagojia ya kiusemezano (Leal, 2015). Hii ina maana kuwa wanafunzi wanapewa nafasi ya kushiriki kimazungumzo katika usomaji wao.

Mbinu hii inalenga katika kuwahamasisha wanafunzi kuwa makinifu (critical thinking). Ili kufikia lengo hili, ni muhimu kujenga mazingira yaliyo tulivu kwa kuondoa wasiwasi wowote pamoja na kuteua mada ambazo hazitazua mabishano darasani. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi hawatachukua muda mrefu wakijadili mambo yaliyo nje ya somo, ni vizuri mwalimu kuwa na mpangilio maalum. Kuwa na mpangilio ni muhimu kwa sababu unachangia katika matumizi ya lugha ya kimazungumzo na kimaandishi. Leal, (2015:204) anapendekeza mpangilio ufuatao:




Mpangilio wa majukumu Kutoka Leal (2015: 204)

Kwa mujibu wa Potyaeva (2005), Ngugi (2012) na Leal (2015) zipo mbinu kadha wa kadha ambazo zimependekezwa na wataalamu wa fasihi ya watoto na ambazo walimu wanaweza kuzishirikisha katika somo la fasihi na wanafunzi wao. Mbinu hizi zinaweza kutumika kabla ya usomaji, wakati wa kusoma na baada ya kusoma.

| **Kabla ya usomaji** | **Wakati wa kusoma** | **Baada ya kusoma** |
|---|---|---|
| • Utoaji wa maoni<br>• Ujengaji wa matarajio | • Kusoma kwa sauti<br>• kutunga nyimbo | • Mbinu za ufahamu<br>• Kutoa mahitimisho |

| | | |
|---|---|---|
| • ubashiri wa mwisho wa hadithi<br>• Uonyeshaji vielelezo<br>• Utoaji mifano<br>• kufikiri kwa sauti<br>• kuuliza maswali na kujadili<br>• kuteua kitabu cha kusoma<br>• Usomaji wa kujitegemea | kutokana na hadithi<br>• kuelekeza katika usomaji<br>• kuwa na wakati wa kutulia na kufikiria<br>• kusoma – kutulia – kujadili<br>• kutalii kila sura ya hadithi<br>• Msomaji Kujitathmini<br>• kuwaza na kujenga taswira<br>• kusikiliza na kusoma<br>• Usomaji kimakundi | • kurejelea makala na kuwa na ufahamu wa awali wa mambo<br>• kujifunza mbinu za mpangilio wa Makala<br><br>• Kukuza lugha<br>• kuhimiza mbinu za kutafakari<br>• Kuhimiza ubunifu |

Mbinu za kuendeleza na kuimarisha usomaji

Kutoka Ngugi (2011: 91)

**Mbinu za Kuendeleza somo la Fasihi**

Mpangilio wa somo la fasihi unaweza kufanyika katika awamu mbalimbali kama inavyopendekezwa na Leal (2015):

Jedwali 1. Mpangilio wa somo

---

**Awamu ya 1.** Ujeuri wa Mbwa (Pamela M. Ngugi)

Mwalimu na wanafunzi kuchukua hatamu ya kusoma aya moja moja ya hadithi kwa sauti

.......................................................................

Wanafunzi kutambua maneno wasiyoyajua / magumu kutoka kwa hadithi. Wayaandike maneno hayo vitabuni

Wanafunzi wanaofahamu maana ya maneno hayo wahimizwe kuyaeleza kulingana na yalivyotumiwa katika hadithi.

.......................................................................

Andika batli ya msamiati (*Vocabulary log*)

.......................................................................

Wakitumia msamiati mpya, wanafunzi wabuni na kujadili maswali ya kiutambuzi

Makundi kujadili maswali miongoni mwao

Maswali yajadiliwe darasani.

.......................................................................

Zoezi la **Mhusika Ninayempenda**

Toa sababu za kumpenda mhusika huyu na uchore picha yake.

............................................................................

**Uandikaji upya wa sarufi,** wanafunzi waandike upya aya ya kwanza ya hadithi

Wabadilishe vitenzi kutoka wakati uliopita hadi wakati uliopo / Watathmini kazi za wenzao katika kikundi.

==========================================

**Awamu ya 2** Unajua ni Kwa Nini? (Pamela Ngugi)

Wanafunzi kuchukua hatamu ya kusoma aya moja moja ya hadithi kwa sauti

............................................................................

Wanafunzi kutambua maneno wasiyoyajua / magumu kutoka kwa hadithi

Wayaandike maneno hayo vitabuni

Wanafunzi wanaofahamu maana ya maneno hayo wahimizwe kuyaeleza kulingana na yalivyotumiwa katika hadithi.

............................................................................

Andika batli ya msamiati (Vocabulary Log)

............................................................................

Ukitumia msamiati mpya, wanafunzi wabuni na kujadili maswali ya kiutambuzi

Makundi kujadili maswali miongoni mwao

Maswali yajadiliwe darasani.

..............................................................................

**Uandikaji upya wa sarufi,** wanafunzi waandike upya aya mbili za mwisho za hadithi

Wabadilishe vitenzi kutoka wakati uliopita hadi wakati ujao/ Watathmini kazi za wenzao katika kikundi.

==========================================================

**Awamu ya 3. Kulinganisha na kulinganua hadithi.**

Kuna mfanano gani katika hadithi hizi?

Wakiwa kwa makundi, wanafunzi wajaze jedwali la mfananisho

..............................................................................

**Kutathmini Msamiati /kitabu cha mazoezi**

Wakiwa kwenye makundi, waunde sentensi nyingi iwezekanavyo katika muda mfupi wakitumia orodha ya msamiati.

---

**Awamu ya 4 Usimulizi mpya wa** Ujeuri wa Mbwa / Unajua ni kwa nini?

Mwanafunzi ateue kati ya kuandika hatima tofauti ya hadithi au aandike hadithi kwa kuegemea kwa mtazamo wa mhusika.

..............................................................................

**Wanafunzi wasimuliane hadithi walizoziandika. Kisha wahojiane kwa kuuliza maswali ya kitathmini na kuandika majibu ya wenzao kwenye kitabu chao.**

Hafiz, Z. A. (2002). Children's literature and language learning. IPBA International Conference Proceedings. Kuala Lumper.

Hiebert, E.H. & Colt, J. (1989). Patterns of literature-based reading instruction. The Reading Teacher, 43. kr. 14-20.

Hillel, M., & Mappin, A. (1995). Choosing and Using Literature. Melbourne: Curriculum Corporation.

Hillman, J. (1999). Discovering children's literature (2nd ed.). Upper Saddle River, NJ: Merrill.

Hodder & Stoughton Bottighmier, R. B. (1998). *An important system of its own. Defining children's literature*. Princeton University Chronicle, 2, 190-210.

Hollindale, P. (1997). *Signs of childness in children's books*. Stroud: Thimble. Houia.

Huck, C. S., Helper, S., Hickman, J., & Kiefer, B. Z. (2001). *Children's Literature in the Elementary School*. New York: The McGraw-Hill Companies, Inc.

Hunt, P. (1996). Defining children's literature and children. In P. Hunt (Mh.), *International Companion Encyclopaedia of Children's Literature*. London: Routledge.

Jalongo, M. (2004). *Stories that teach life lessons*. Scholastic Parent & Child, 12(2), 36-42.

Kembo J. (2016). "The Challenges of teaching in a foreign Language: An Alternative approach to developing fluency in the language of Instruction" Katika: Calvin Kayi (Mh.) Chemchemi. International Journal of Humanities and Social Sciences. Kenyatta University. Kr.19 -36.

Leal, P. (2015) Connecting reading and writing using children's literature in the university L2 classroom. Katika: Reading in a Foreign Language Juz .27, Na.2

Lesnik-Oberstein, K. (1996). Defining children's literature and childhood. Katika: P. Hunt (Mh.), International

companion encyclopedia of children's literature (pp. 17- 31). London: Routledge.

Lesnik-Oberstein, K. (1999). What is Children's Literature? What is Childhood? Katika: P. Hunt (Mh.), Understanding Children's Literature (pp. 15-29). London: Routledge.

Lowe, D. F. (2009). Helping children cope through literature. Forum on Public Policy Online, 2009(1)

Lukens, R. J. (1995). *A critical handbook of children's literature*. New York: HarperCollins. Kr.199-218.

McDowell, M. (1973). Fiction for Children and Adults: Some essential differences. Children's Literature in Education, 10, 50-53.

Miller, C. R. (1984). "Genre As Social Action." *Quarterly Journal of Speech* 70: 151-67.

Ngugi, P.M. (2012). "Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati." Katika: Shani Omari and George Mrikaria (wah.) *Mulika.* Journal of the Institute of Kiswahili Studies TATAKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juz. 31.2012. Kr. 12-36

Ngugi, P. M.Y. (2014) "Use of Children's Literature in Multilingual Education in Kenya" Katika: *Multilingualism and Education in Africa*: The State of the Art. Katika: Daniel O. O. Orwenjo, Martin C. Njoroge, Ruth W. Ndung'u and Phyllis W. Mwangi (Wah.). New Castle: Cambridge Scholars Publishing. Kr. 102 -117.

Ngugi, P.M (2014) "Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto Kisaikolojia." Katika: D.P.B. Massamba na L.H. Bakize (Wah.) *Kiswahili.* Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Chuo kikuu cha Dar es Salaam Juz. 77.2014. Kr. 170- 180.

Ngugi, P.M.Y. (2016). “Mikakati ya uchambuzi wa Fasihi ya Watoto: Mtazamo wa Upokezi wa Msomaji,” katika D.P.B. Massamba na L.H. Bakize (wah.). Kiswahili, Juz. 79. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Kr. 43 - 52.

Norton, D. (1999). *Through the eyes of a child* (Toleo 5) Englewood Cliffs, NJ: Merrill.

Oittinen, R. (2008). Audiences and Influences: Multisensory Translations of Picturebooks. Katika: Maria Gonzalez & Riita Oittinen (Wah.). *Whose Story? Translating the Verbal and visual in Literature for Young Readers*. Cambridge Scholars Publishing. Newcastle. Kr. 1-18.

O'Sullivan, S. (2004). Books to live by: Using children's literature for character education. Reading Teacher, 57(7), 640-645.

Pennell, C. (2014). In the age of Reading: Understanding Reader’s Engagement with Text, Katika: *The Reading Teacher*. Juz. 6. Na. 4. International Reading Association. Kr. 251-260.smith

Puurtinen T. (1998). Syntax, Reading and Ideology in Children’s Literature. In: Meta: Translators’ Journal, Juz. 43, Na. 4. Kr. 524-533.

Potyaeva, T. 2005. On the way to changing the future. Katika: Gerry Shiel (Mh.). *Proceedings of the 14th European Conference on Reading, Zagreb, Croatia*. Croatian Reading Association. Kr. 345-347.

Prestwich, D. L. (2004). Character education in America's schools. School Community Journal, 14(1), 139-150.

Republic of Kenya, (2017). Basic Education Curriculum Framework. Nairobi. Kenya Institute of Curriculum Development (KICD).

Rosenblatt, L. (1995). (First published 1939). Literature as Exploration. New York: The Modern Language Association of America.

Saxby, H. M. (1997). *Books in the life of a child: bridges to literature and learning*. South Melbourne: Macmillan Education Australia.

Smith-D'Arezzo, W. M., & Moore-Thomas, C. (2010). Children's perceptions of peers with disabilities. TEACHING Exceptional Children Plus, 6(3), 1-16.

Stewig, J. W. (1980). *Children and Literature.* Chicago: Rand.

Tomlinson, C. M., & Lynch-Brown, C. (1996/2002). *Essentials of Children's Literature*. Boston: Allyn and Bacon.

Tunnell, M.O. & Jacobs, J.S. (1989). Using "real books": Research findings on literature-based reading instruction. Katika: The Reading Teacher, 42. International Reading Association. Kr. 470-477.

Uwezo –Kenya, (2016). Are Our Children Learning? Uwezo Kenya Sixth Learning Assessment Report. Nairobi: Twaweza East Africa.

Weinreich, T., & Bartlett, D. (2000). *Children's Literature: art or pedagogy?* Roskilde University Press.

Widdowson, H. G. (1983). Talking shop: On literature and ELT. In *English Language Teaching Journal*, *37* (1), Kr. 30-35.

Winch G., Johnston. R. R., March P., Ljungdahl L., & Holliday M. (2004). *Literacy Reading, writing, and children's literature*. Melbourne: Oxford University Press.

Zarillo, J. (1989). Teachers' interpretations of literature-based reading. In: The Reading Teacher, 43.Kr. 22-29